**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKASHULE YA SEKONDARI NDOMBA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIAOFISI YA**

**WAZIRI MKUU - TAMISEMI**

**Mkuu wa Shule 0752619660/0784493331**

**Shule ya Sekondari NDOMBA,**

**S.L.P. 83,**

**NGARA**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ............................................**
**S.L.P .....................**

Yah**: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI NDOMBA MWEZI …………………….**

1. Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato chaTano katika Shule hii mwaka ………… na atasoma tahasusi ya **HGL/HGK/HKL**

Shule ya Sekondari NDOMBA ipo Wilaya ya Ngara, Mkoa wa Kagera, umbali wa Kilometa 32 Kusini Magharibi mwa Mji wa NGARA. Usafiri kutoka mji wa NGARA unapatikana katika kituo cha mabasi NGARA, nauli ni Shilingi 7000 mpaka shuleni.Kama unatokea Mwanza panda mabasi ya Zube au Nyehunge utashukia **SHULENI**. Kwa wanaotokea mikoani, waje mpaka Kahama, kasha wapande magari ya Kahama-Ngara au Kahama-Rulenge. Shule ipo barabara kuu ya Ngara-Rulenge na ipo karibu na mji mdogo wa Rulenge.

Muhula wa Masomo unaanza ………., hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni mapema kabla ya tarehe ya mwisho.

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 Sare za Shule

i. Sare ya shule hii ni suruali za rangi ya DARK BLUE pea mbiliza kushona( KITAMBAA KIZITO CHA ORIGINAL) Mshono wa marinda mawili na turn up (**SURUALI MTEPESHO/ZILIZOBANA HAZITAPOKELEWA.)**
ii. Shati mbili za rangi nyeupe zenye mikono mirefu yenye vishikizo vya kawaida na zilizowekewa alama ya namba Tano ya kirumi mabegani. Alama hiyo inawekwa kwa KITAMBAA Cha rangi ya DARKBLUE.
iii. Sare ya Michezo ni jezi ya rangi ya Nyeupe ( T-Shirt na bukta yake) pamoja na track suit za rangi nyekundu, raba za michezo na soksi ndefu rangi nyekundu.
iv. Viatu vya shule ni vyeusi vya kufunga na kamba vyenye visigino vifupi na visiwe buti.
v. Soksi jozi tano dark blue
vi. Sweta moja nyeusi itawekewa nembo ya shule. Ukiipata njoo nayo itawekewa nembo hapa shuleni, usipoipata shule itatafuta mzabuni mmoja ili ziweze kufanana kwa gharama ya Tsh 15,000/=
vii. Nguo za kushindia (*shamba dress*) ni suruali mbili za rangi ya damu ya mzee KITAMBAA kizito na T-shirt 2 rangi ya damu ya mzee zenye kola. Ukiweza kuipata njoo nayo itawekewa nembo hapa shuleni, usipoipata zipo zitakazoagizwa kwa mzabuni wa shule zikiwa na nembo ya shule tayari kwa T.sh 15,000=
viii. Tai Moja dark blue (itawekewa nembo ya shule)

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

i. Madaftari makubwa ( counter books) tano.
ii. **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) kwa mwaka kwa ajili test za mara kwa mara. Aina ya ream ni DOUBLE A

iii. Vitabu vya masomo ya tahasusi husika ( riwaya,tamthiliya na ushairi). Kwa wanafunzi wa masomo ya Lugha, Advanced learners dictionary na kamusi ya Kiswahili ni vitabu vya muhimu sana mwanafunzi kuwa navyo.

iv. Scientific Calculator kwa wanafunzi wa Geography

v. Godoro la futi mbili na nusu (2 1/2).

vi. Mashuka Jozi 2 rangi ya pink, blanket 1, foronya ya godoro1, chandarua 1 rangi nyeupe , Taulo ya kuogea

vii. Nguo za ndani za kutosha;

viii. Vyombo vya chakula (sahani, bakuli, kijiko na kikombe chabati);

ix. Ndoo 1 kubwa yenye mfuniko rangi ya kijani,dumu la lita 5 rangi nyeupe kwa ajili ya kutunzia maji ya kunywa na beseni 1 rangi ya kijani.

x. **HGL**- Aje na kwanja 1, squizer 1, jembe 1 na mpini wake na sabuni ya maji Lita 5

**HKL**- Aje na jembe 1 na mpini wake, mfagio wa ndani 1(hard bloom), kotama 1 na sabuni ya maji Lita 5.

**HGK -** Aje na kotama 1, mfagio wa ndani (soft bloom) 1, jembe 1na mpini wake na sabuni ya maji Lita 5.

xi. Tochi/taa kwa ajili ya matumizi ya dharura

xii. Vifaa vingine muhimu kwa matumizi binafsi kama vile mswaki,dawa ya viatu,sabuni,mafuta ya kupaka,n.k.

xiii. Bima ya Afya (LAZIMA)

xiv. Sanduku moja la mbao kwa ajili ya kutunzia vitu vyake.

## 1.1 Michango mbalimbali

**Shule za Bweni**

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Mchango wa Uendeshaji wa Shule | 65,000/= |
| 3. | Tahadhari | 5,000/= |
| 4. | Nembo za mashati mawili | 5,000/= |
| 5. | Kitambulisho cha Shule | 5,000/= |
| | **Jumla** | **80,000/=** |

**Michango ilipwe kupitia akaunti ya shule ifuatayo**

**JINA: NDOMBA SECONDARY SCHOOL**
**AKAUNTI: 32101200065**
**BENKI: NMB**

## 2. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha,inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Waziri Mkuu - TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi nautapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 2.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shulekulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kikamilifu masomo ya usiku (night Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya shule wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule na binafsi;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari.

**MUHIMU:**

- **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**

- **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku**

**mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au ugojnwa)**.

**2.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa za utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtuyeyote yule;
vi. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kusababisha mimba;
xii. Kushiriki matendo ya uhalifu na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiii. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xiv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira yashule;
xv. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvi. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xvii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

## 3. Viambatisho na Fomu Muhimu

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wakutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;

iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule.
iv. Picha nne(4) (passport size) ya mwanafunzi.
v. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zaoza Simu.
vi. Bima ya Afya.

**NDOMBA TUNAAMINI KUWA UTAPATA ELIMU BORA NA KUWA MTU SAHIHI KWA JAMII YA KITANZANIA.**

**NDOMBA BILA DARAJA LA TATU, NNE NA SIFURI INAWEZEKANA, KARIBU UTIMIZE WAJIBU WAKO NA KUKAMILISHA NDOTO YAKO**

Tafadhali soma kwa makini maelezo / maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA SHULE YA SEKONDARI NDOMBA**

**.....................................**
**ONESMO EMMANUEL BULINDORI**
**MKUU WA SHULE**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu nakuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika ambaye ni mwanafunzi nimgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUSU MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WASHULE ILI KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule 0752619660/0784493331**
- **Makamu Mkuu wa Shule 0756259656**
- **Mwandamizi Taaluma 0768058070**

**SHULE YA SEKONDARI NDOMBA**

**FOMU YA KUANDIKISHWA**

**SHULE**

***(Ijazwe kwa herufi kubwa na kurejeshwa kwa mkuu wa shule)***

i. Jina kamili (mwanafunzi) ……………………………………………………….
Tarehe ya kuzaliwa …………………..... Wilaya ……………….. Mkoa…………..........
Taifa..................................... Dini RC/Anglican/Lutheran/Muslim/Pentecosten.k
Shule ya SEKONDARI unayotoka…………………………………………....

ii. Jina kamili la Baba/Mama/Mlezi ……………………………………………….
Anwani yake……………………………………………………………………..
Kazi ya baba/Mama/Mlezi……………………………………………………....
Anwani yake……………………………………………………………………
Namba ya simu…………………………………………………………………..

**AHADI YA MWANAFUNZI.**

i. Mimi .........................................................................................nimeyasoma na Kuyaelewa maelezo yote ambayo ni pamoja na sheria na kanuni za shule ni nimekubali kuingia kidato cha TANO katika shule ya Sekondari Ndomba kuanzia Tarehe.............. hadi nitakapomaliza kidato cha SITA .

ii. Kwa hiyo naahidi kwamba:-
   (a) Nitazitii sheria zote za shule na kutimiza mambo yote muhimu yaliyotajwa.
   (b) Sitashiriki katika vitendo vya hujuma wala vitendo ambavyo vitakuwa kinyume na uongozi wa shule na serikali ja Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kama kushiriki migomo ,Fujo,makosa ya jinai n.k.
   (c) Nitatunza mali za UMMA ambazo ni pamoja na majengo na samani,vitabu n.k
   Tarehe ……………………... Sahihi ya mwanafunzi………………………

**AHADI YA MZAZI/MLENZI**

Mimi …………………………………….... ambaye ni mzazi/mlenzi wa mwanafunzi ……………………………………………….. nina ahidi kwamba :-

i. Nitashirikiana na uongozi wa shule , walimu na watumishi wasowalimu katika kuhakikisha mwanangu anatii sheria na kanuni za shule ya sekondari Ndomba iwapo atashindwa kutii sheria hizo nitalazimika kukubaliana na adhabu itakayotolewa na uongonzi wa shule.

ii. Nitafanya kila niwezalo kuwezesha mwanangu kusoma kwa bidii kama ilivyoelekezwe na shule.

Sahihi…………………………………Tarehe……………………………
Namba ya simu……………………………………………………………..

NGARA DISTRICT COUNCIL

NDOMBA SECONDARY SCHOOL

**MEDICAL EXAMINATION**

To be completed by Medical officer in respect of Ndomba Secondary School student.(entrant)

2) Student's full name…………………………………………………………..
3) Sex……………………………………………......................................
4) HGB Test…………………………………………………………………..
5) STOOL Test: ……………………………………….............................
6) URINE……………………………………………………………………….
7) T.B Test: …………………………………………..............................
8) EYE Examination:…………………………………………………………..
9) E.N.T …………………………………………………………………..
10) CHEST……………………………………………………………………
11) ABDOMEN ……………………………………………………………

ADDITIONAL INFORMATION

Physical defects or impairments, infection, chronic or hereditary (family disease).

…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

I certify that I have examined the above student and discover that HE/SHE is Physically /NOT physically fit for further studies .

NAME : …………………………………………………………..

SIGNATURE……………………………………………………..

DATE: ……………………………………………………………

**OFFICIAL STAMP**